#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo No. 9

Januari - Machi 2023



## RAIS DKT. SAMIA

## APANDISHA POSHO YA WANAFUNZI HADI TZS 10,000

**Na Mwandishi Wetu,**
**Dodoma**

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa wanafunzi wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kukumbuka kurejesha mikopo hiyo mara watakapohitimu masomo yao ili iweze kunufaisha wanafunzi wengine.

Rais Samia ameyasema hayo Februari 11, 2023 wakati alipokuwa akizungumza na Shirikisho la Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) na Shirikisho la Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZAHILFE), Ikulu Chamwino, Jijini Dodoma.

"Mnaonufaika na mikopo ya elimu ya juu mkipata kazi rudisheni ili na mdogo wako na yeye asome, sasa mkisoma mkatoka, mkaenda … sio uzalendo wala hamtendi haki", amesema Dkt. Samia.

Aidha, Rais Samia ameiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupandisha posho ya kujikimu ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka TZS 8,500/= hadi kufikia TZS 10,000/= kwa siku na kuongeza kuwa Serikali inafanya jitihada mbalimbali za kuinua elimu ya juu kwa kuongeza fursa za upatikanaji wake na kuwasisitiza wanafunzi hao kuweka mkazo katika masomo na kujiepusha na vitendo viovu.

Kwa upande wake Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amemshukuru Rais Samia kwa kutoa fursa ya kukutana na wawakilishi hao wa wanafunzi wa elimu ya juu na kumshukuru kwa kutoa kipaumbele katika sekta ya elimu ya juu ikiwemo kuongeza bajeti ya mikopo kutoka TZS 570 bilioni mwaka 2021/2022 hadi kufikia TZS 654 bilioni mwaka huu 2022/2023.

> **"Mnaonufaika na mikopo ya elimu ya juu mkipata kazi rudisheni ili na mdogo wako na yeye asome, sasa mkisoma mkatoka, mkaenda … sio uzalendo wala hamtendi haki", amesema Dkt. Samia.**

Aidha Waziri Mkenda amemuahidi Mheshimiwa Rais kuwa Wizara na Taasisi zinazosimamia elimu ya kati na juu zitaongeza ushirikishwaji wa serikali za wanafunzi kwa kuweka mfumo utakaorahisisha mawasiliano baina yao.

Kwa upande wake Rais wa TAHLISO, Frank Nkinda amempongeza Rais Samia kwa kuendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwenye vyuo vya elimu ya juu kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) pamoja na kuondoa 6% ya tozo ya kutunza thamani ya mkopo na 10% ya adhabu ya kuchelewa kuanza kurejesha mkopo wa elimu ya juu.

Nkinda ameshukuru na kupongeza ushirikiano wa kipekee wanaoupata kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Kikao cha Mheshimiwa Rais na viongozi wa Shirikisho la Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu pia kilihudhuriwa na watendaji wa Taasisi zinazohusika na Elimu ya Juu akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru.

## JAMBO LETU



**Ismail Ngayonga**
*Mhariri*

## MAMA KASEMA "TUREJESHE MIKOPO YA ELIMU YA JUU ILIYOIVA"

Urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu ni suala endelevu linalolenga kuhakikisha waliokopeshwa kwa ajili ya masomo ya ngazi hiyo ya juu kielimu wanarejesha fedha za mikopo yao iliyoiva ndani ya muda unaokubalika.

Urejeshaji mikopo ya elimu ya juu siyo tu kwamba ni suala la kisheria kama linavyotajwa katika Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu SURA 178 lakini pia ni kuonesha uzalendo na kuwajali watanzania wengine wahitaji wanaoingia elimu ya juu.

Katika mkutano kati ya Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan na Viongozi wa Shirikisho la Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Juu (TAHLISO) uliofanyika Ikulu ya Chamwino, Jijini Dodoma Februari 11, 2023, pamoja na kusikiliza hoja mbalimbali kuhusu masuala muhimu ya mikopo kwa wanafunzi wanaonufaika na wanaoendelea na masomo mwaka huu likiwemo ombi la kuongezewa kiasi cha fedha za kujikimu kwa siku; Mheshimiwa Rais alitoa rai kwa walionufaika kurejesha mikopo hiyo.

Kauli ya Mheshimiwa Rais imekuja akitambua umuhimu wa kusomesha vijana watanzania walio wengi katika ngazi ya elimu ya juu ili kupata wasomi na wataalam katika nyanja mbalimbali na hivyo kuiwezesha nchi yetu kupiga hatua kimaendeleo.

Itakumbukwa kuwa mwaka 2021 katika Sherehe za Siku ya Kimataifa ya Wafanyakazi; Mei Mosi zilizoadhimishwa Jijini Mwanza, pamoja na kutangaza ahueni katika urejeshaji mikopo ya elimu ya juu kwa kuondoa Tozo ya Kulinda Thamani ya Mikopo (VRF), alitumia fursa hiyo kuwahimiza walionufaika kuendelea kurejesha mikopo yao.

Katika kipindi cha miaka miwili madarakani, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameonesha nia na dhamira ya kuimarisha ugharimiaji wa elimu ya juu kwa kuongeza bajeti ya mikopo kutoka TZS 464 bilioni mwaka 2020/2021 hadi TZS 570 bilioni mwaka 2021/2022 na mwaka huu 2022/2023 imefikia TZS 654 bilioni ambayo imewezesha wanafunzi zaidi ya 200,000 kunufaika, miongoni mwao wanafunzi 72,979 ni wa mwaka wa kwanza.

HESLB inawapongeza wanufaika mmoja mmoja wanaozingatia na kurejesha mikopo yao mara baada ya kuiva. Pongezi pia kwa waajiri wa wanufaika kwa kushirikiana na Serikali kupitia HESLB kusimamia urejeshaji wa mikopo kwa kuwasilisha majina ya waajiriwa wapya, kukata na kuwasilisha makato ndani ya siku 15 ya mwezi unaofuata.

Fedha zinazorejeshwa zinawezesha kuunga mkono jitihada za Serikali katika kugharimia elimu ya juu kwa wanafunzi wahitaji kwa kuongeza kiasi cha fedha kwenye bajeti ya mikopo ya wanafunzi kila mwaka. Katika mwaka wa masomo 2022/2023 kiasi cha fedha za mikopo kilichoidhinishwa ni TZS 654 bilioni; sehemu ya kiasi hicho, TZS 183 bilioni zimetokana na makusanyo ya mikopo illiyoiva.

Kwa kuzingatia kwamba mahitaji ya fedha za kugharimia elimu ya juu yanaongezeka kila mwaka kutokana na ongezeko la wanafunzi wanaohitimu kidato cha sita na ngazi za sifa linganishi (Stashahada) wanaopata udahili wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu, ni wazi kasi na kiwango cha fedha za mikopo iliyoiva zinazokusanywa inabidi iongezeke ili kukidhi mahitaji.

Hima wanufaika ambao hamjalipa madeni yenu yaliyoiva jitokezeni mrejeshe ili mumuunge mkono Mheshimiwa Rais.

**NDANI...**



03 **JASPER:** NIMERIDHISHWA NA UTOAJI HUDUMA HESLB



05 **MADINA:** SERIKALI IMENIWEZESHA, NITAOKOA MAISHA YA ....




08 **WAZIRI MHAGAMA:** TUMIENI MIFUMO KUBADILISHANA TAARIFA

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Abdul-Razaq Badru

**Katibu**
Omega Ngole

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Ismail Ngayonga
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Jacqueline Msuya

**Designer**
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Mkurugenzi Mtendaji
Bodi ya Mikopo ya
Wanafunzi wa Elimu ya Juu
1 Mtaa wa Kilimo, TAZARA
S.L.P 76068
Dar es salaam
Tanzania

**Simu:** 0739 665 533
**Barua Pepe:** adcp@heslb.go.tz
**Tovuti:** www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



# KUREJESHA MIKOPO YA ELIMU YA JUU NI UZALENDO

Nakukaribisha tena katika toleo hili la 9 la Jarida la Mtandao HESLB Yako ili kupata habari na matukio yaliyojiri katika robo ya mwaka illiyoishia Machi 31, 2023. Ni wazi mambo mengi yametokea katika sekta ya elimu na hususan katika masuala ya ugharimiaji wa elimu ya juu.

Toleo hili limejikita zaidi katika urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa kutambua kuwa ni sehemu muhimu ya kuhakikisha mfuko wa ugharimiaji wanafunzi wahitaji wanaojiunga na masomo katika ngazi ya elimu ya juu kila mwaka wana uhakika wa kupata mikopo ya kukidhi mahitaji yao kulingana na uhitaji wao.

Mwanafunzi mhitaji anapopangiwa mkopo kisha kuanza safari ya masomo ya elimu ya juu na hatimaye kuhitimu; anatarajiwa kurejesha mkopo huo baada ya kuiva ili marejesho hayo yaweze kusaidia kusomesha wanafunzi wengine wahitaji. Hii ndio maana ya uendelevu wa mfuko wa mikopo ya elimu ya juu.

Ni wazi kila mwaka Serikali inaongeza kiasi cha fedha kwa ajili ya kukopesha wanafunzi ambao idadi yao inaongezeka mwaka hadi mwaka. Hili ni jambo la kupongeza kwa kuwa Serikali inatambua umuhimu wa kusomesha idadi kubwa ya wanafunzi katika ngazi ya elimu ya juu ili kujihakikishia kuwa na wasomi na wataalamu wa fani mbalimbali.

Mwaka huu 2022/2023 Serikali imetumia kiasi cha TZS 654 bilioni kusomesha wanafunzi wapatao 202,016 ikiwa ni ongezeko kubwa zaidi la bajeti na idadi ya wanafunzi walionufaika ikilinganishwa na mwaka 2021/2022 ambapo bajeti ilikuwa TZS 570 bilioni.

Februari 11, mwaka huu katika mkutano kati ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan na Viongozi wa Shirikisho la Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO) na Shirikisho la Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZAHILFE) uliofanyika Ikulu ya Chamwino, Jijini Dodoma, pamoja na Mheshimiwa Rais kuridhia ombi la kuongeza posho ya kujikimu kwa siku kutoka TZS 8,500/= hadi TZS 10,000/= kwa wanafunzi waliopo masomoni, pia alitumia mkutano huo kukumbusha umuhimu wa wanufaika waliohitimu kurejesha mikopo yao.

Rai ya Mheshimiwa Rais katika kikao na viongozi wa TAHLISO na ZAHILFE ni mwendelezo wa tamko kama hilo alilolitoa katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika kitaifa Jijini Mwanza, Mei Mosi, 2021 ambapo pia aliwahimiza walionufaika kutambua umuhimu wa kurejesha mikopo yao na kutangaza kuondoa tozo ya 6% ya kulinda thamani ya mikopo iliyokuwa inaongezwa kwenye salio la deni la mnufaika kila mwaka ili kuwapa hamasa ya kurejesha.

Ni kwa muktadha huo huo, Meza ya Mwenyekiti inaungana na Mheshimiwa Rais kuwakaribisha wanufaika wote ambao madeni yao yameiva na bado hawajaanza kulipa madeni hayo wajitokeze. HESLB imeweka utaratibu rahisi kuwezesha wanufaika kupata ankara (loan statement) za madeni yao na kulipa kupitia kwenye mifumo iliyounganishwa kwenye tovuti yake www.heslb.go.tz.

Uzalendo unapimwa kwa vitendo na kuwa tayari kulilinda na kulitetea taifa lako. Shime wanufaika wote ambao hamjaanza kurejesha mikopo yenu au mmesimama kurejesha kabla ya deni kuisha; jitokezeni mlipe hadi kumaliza madeni yenu kuwezesha watanzania wengine wahitaji nao kunufaika.



# JASPER:
## NIMERIDHISHWA NA UTOAJI HUDUMA HESLB

Na Mwandishi Wetu
Igunga

"Moyo wa shukrani ni ustaarabu kwa aliyenufaika na ni heshima kwa aliyetoa huduma". Hayo ni maneno ya Jasper Mushobozi Tito, Afisa Ardhi anayefanya kazi Wilaya ya Igunga mkoani Tabora ambaye pia ni mnufaika wa mkopo wa elimu ya juu.

Jasper, mhitimu wa Shahada ya Ualimu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (2011-2014) na kisha Shahada ya Sheria (2020) kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, alituma barua pepe kutoa neno la shukrani kwa HESLB baada ya kurejeshewa kiasi kilichozidi cha marejesho ya mkopo wake.

Katika barua pepe hiyo Jasper aliandika akieleza kuwa anakosa neno la shukrani zaidi ya ahsante kutokana na jinsi alivyohudumiwa kwa weledi na watumishi wa HESLB tangu alipowasilisha ombi lake la kurejeshewa fedha za ziada alizolipa baada ya kumaliza deni lake hadi alipolipwa fedha hizo.

Akisimulia ilikuwaje akalipa zaidi ya kiasi cha mkopo aliokuwa anadaiwa, Jasper anasema, "nilikopa fedha kutoka Benki fulani ili kulipa salio la deni langu la HESLB lakini baada ya kuwa nimemaliza kulipa deni lote kwa bahati mbaya mwajiri wangu aliendelea kunikata… niliamua kuwasiliana na HESLB kuhusu kukatwa zaidi na kisha wakanipa utaratibu wa kuwasilisha ombi langu kwa njia ya mfumo (portal). Nashukuru nililipwa kiasi chote kilichokuwa kimezidi baada ya uhakiki kukamilika".

Pamoja na kupongeza kutokana na kuridhishwa na utoaji huduma wa maafisa wa HESLB, Jasper anatamani taasisi nyingine za umma ziige mfano huo wa kutoa huduma kwa haraka, weledi na ufanisi hali anayoielezea kuwa, "mimi pia imenipa morali ya kuhudumia vizuri wateja wanaofika kupata huduma ofisini kwangu", anasisitiza Jasper.

Jasper anawaasa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu ambao madeni yao yameiva na wangependa kuanza kurejesha madeni hayo watembelee tovuti ya HESLB www.heslb.go.tz kisha kubofya kipengele cha Loan Repayment ili kupata ankara na taarifa za madeni yao.

Njia ya kutumia mtandao inaokoa muda na kurahisisha wanufaika kulipa au kufuatilia mwenendo wa urejeshaji wa fedha za madeni yao bila usumbufu.


> **"nilikopa fedha kutoka Benki fulani ili kulipa salio la deni langu la HESLB lakini baada ya kuwa nimemaliza kulipa deni lote kwa bahati mbaya mwajiri wangu aliendelea Kunikata ...niliamua kuwasiliana na HESLB kuhusu kukatwa zaidi na kisha wakanipa utaratibu wa kuwasilisha ombi langu kwa njia ya mfumo (portal). Nashukuru nililipwa kiasi chote kilichokuwa kimezidi baada ya uhakiki kukamilika"**




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi Omari Dihenga (wa nane kulia) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya ZHELB Prof. Mohammed Hafidh Khalfan (wa pili kushoto) katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru (katikati) na Mkurugenzi Mtendaji wa ZHELB Iddi Khamisi Haji (wa tatu kulia) ambaye pia ni mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB katika picha ya pamoja na ujumbe kutoka NAMA Foundation ya Malaysia, Africa Education Development Trust ya Saudi Arabia/Kenya na Tanzania Education Development Trust ya Tanzania. Wengine katika picha ni maafisa waandamizi wa HESLB na NAMA. Kabla ya kutembelea HESLB Februari 1, 2023, Ujumbe huo ulipokelewa na kufanya majadiliano na Menejimenti ya ZHELB. Ujumbe kutoka Malaysia uliongozwa na Mkurugenzi Mtendaji NAMA Foundation Dkt. Saleh Mubarak Bazead (wa tatu kushoto).




Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Kenya (HELB), CPA Charles Ringera (kushoto) akipeana zawadi na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul Razaq Badru wakati ujumbe wa watumishi wa HESLB ulipotembelea HELB Jijini Nairobi kwa ziara ya mafunzo ya siku 4 kuanzia Februari 28 hadi Machi 3, 2023.




Mgeni rasmi katika Kongamano la Ugharimiaji wa Elimu ya Juu Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), Dkt Franklin Rwezimula (katikati) akiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi O. Dihenga (kulia kwake) na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya ZHELB Prof. Mohammed Hafidh Khalfan (kushoto kwake). Wa Kwanza kushoto ni Mkurugenzi wa Elimu ya Juu (WyEST) Dkt Kennedy Hosea na wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru. Kongamano hilo lililofanyika Jijini Dodoma Machi 16, 2023 chini ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), lilijumuisha wadau wa ugharimiaji wa elimu ya juu kutoka Wizara, vyuo vikuu, taasisi za fedha na mashirika yasiyo ya serikali ya Tanzania Bara na Zanzibar.





Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul-Razaq Badru (wa tatu kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa SATF, Beatrice Mgaya (wa nne kulia) wakiwa na watumishi wa taasisi hizo mbili katika picha ya pamoja mara baada ya kusaini makubaliano ya kuhakikisha wanafunzi wahitaji wanaotoka katika kaya maskini au mazingira magumu waliofadhiliwa na SATF wanapata udahili na mikopo ya kugharimia elimu ya juu nchini. Makubaliano baina ya HESLB na SATF yalisainiwa Januari 31, 2023 katika ofisi za SATF jijini Dar es salaam.




Ujumbe wa watumishi wa HESLB wakiongozwa na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt Kennedy Hosea (wa pili kushoto) katika picha ya kumbukumbu baada ya ziara ya mafunzo katika Bodi ya Udhamini wa Mikopo ya Wanafunzi nchini Ghana iliyofanyika Februari 19 -25, 2023 kwa lengo la kupata uzoefu katika utoaji na urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu.




Watumishi wa HESLB katika picha ya pamoja baada ya kutembelea Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Kenya (HELB). Watumishi hao wa HESLB walitembelea HELB Jijini Nairobi kwa ziara ya mafunzo ya siku 4 kuanzia Februari 28 hadi Machi 3, 2023 kujifunza mbinu za kisasa za kuhudumia wateja katika utoaji na urejeshaji mikopo ili kuboresha ufanisi.



# MADINA:

## SERIKALI IMENIWEZESHA, NITAOKOA MAISHA YA WATANZANIA

**Na Mwandishi Wetu**
**Dar es Salaam**

Madina Hassan Mwevi, binti mwenye umri wa miaka ishirini na mmoja (21), mwanafunzi wa mwaka wa kwanza wa Shahada ya Udaktari katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU) kilichopo Jijini Dar es Salaam anaishukuru serikali kwa kumwezesha kuendelea kusoma kupitia mkopo wa elimu ya juu ili atimize ndoto zake za kuwa daktari na kusaidia watanzania wengine.

Akiongea na jarida hili, Madina anasema aliamua kusomea shahada ya Udaktari ili aweze kuokoa maisha ya watanzania kwa kuwatibu pale wanapokumbana na maradhi na kuwapa ushauri sahihi kuwawezesha kuwa na afya njema.

"Baba yangu alikuwa ni daktari, bahati mbaya alifariki mwezi Machi, 2022 nikiwa kidato cha sita…Nilikuwa nikipenda sana udaktari na niliamua kusomea taaluma hii ili na mimi niweze kuwasaidia watu wengine wanapopatwa na maradhi", anaelezea Madina.

Aidha, Madina amesema kwa sasa mtu pekee anayemtegemea ni mama yake mzazi ambaye anajishughulisha na biashara ndogo ya kuuza mkaa ili kupata kipato cha kuihudumia familia yake.

Madina anaishukuru serikali kwa kumwezesha kupata mkopo akibainisha kuwa bila mkopo huo huenda asingeweza kujiunga na elimu ya juu na kuendelea na masomo hayo ya Udaktari aliyokuwa anayatamani.

"Niliipoomba mkopo awali nilipata ada kiasi cha shilingi laki sita na elfu hamsini (650,000) tu. Mwanzoni nilikata tamaa maana niliona mama hataweza kuongezea kiasi kilichobaki ili nisome…Naishukuru sana Bodi ya Mikopo maana walipofungua dirisha la kukata rufaa, nikaomba kuongezewa mkopo kupitia rufaa na nimefanikwa kuongezewa ada hadi kufikia shilingi milioni tatu na laki moja (3,100,000)", amesema Madina.

Kwa upande mwingine, Madina ameiomba Serikali iendelee kutoa kipaumbele kwenye mikopo ya elimu ya juu kwa makundi ya wahitaji kama vile yatima, walemavu na wanafunzi wanaotoka kwenye kaya zisizokuwa na uwezo wa kugharimia watoto wao kuweza kupata elimu ya juu.

Madina ni miongoni mwa mabinti wa kitanzania wanaowezeshwa na Serikali kupitia mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Mwaka huu 2022/2023, Serikali imetoa mikopo yenye thamani ya TZS 654 bilioni kwa wanafunzi 202,016 kati yao wanafunzi 72,979 ni wa mwaka wa kwanza.



# HESLB, WADAU WATATHMINI MIKOPO KUJIANDAA MSIMU UJAO

Na Mwandishi Wetu
Zanzibar

HESLB imefanya kikao kazi cha tathmini ya zoezi la uombaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2022/2023 ili kujipanga kwa msimu ujao wa 2023/2024.

Kikao hicho kilichokutanisha wadau wa kimkakati katika mnyororo wa uombaji mikopo kilifanyika Machi 9, 2023 Unguja, Zanzibar na kuhudhuriwa na wadau wa HESLB wakiongozwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB), Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Taasisi ya Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA), Shirika la Posta Tanzania (TPC) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Taasisi nyingine zilikuwa Shirikisho la Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO), Shirikisho la Wanafunzi wa Elimu ya Juu Zanzibar (ZAHILFE), Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA) pamoja na Social Action Trust Fund (SATF).

Kufanyika kwa kikao kazi hicho kuliwezesha washiriki kutaja mafanikio na kubainisha changamoto zilizojitokeza katika kipindi kilichopita cha uombaji wa mikopo ambapo jumla ya waombaji mikopo zaidi ya 90,000 walituma maombi yao, na kati yao wanafunzi 72,979 wa mwaka wa kwanza walipangiwa mikopo. Aidha wadau hao pia walipata fursa ya kutoa maoni na mapendekezo ya jinsi ya kutatua changamoto zilizojitokeza katika msimu uliopita na kuweka maazimio ya mafanikio bora ikiwa ni maandalizi ya msimu wa mwaka wa masomo 2023/2024.

ZAHILFE ni moja ya taasisi zilizotoa pongezi kwa HESLB na ZHELB kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kuwahudumia wanafunzi wa vyuo vikuu vya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kwa upande wake Rais wa TAHLISO Frank Nkinda aliishukuru HESLB kwa namna inavyoshughulikia kwa haraka masuala ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na kushauri kuendelea kushauriana na wadau mbalimbali wa elimu ili kuboresha mifumo ya kukabiliana na changamoto za wanafunzi kwa mwaka ujao wa masomo.

Sambamba na hilo TAHLISO imetoa ahadi ya kuendelea kushirikiana na Taasisi na wadau wa elimu ili kuimarisha uhusiano mwema na utendaji kazi katika kutoa huduma bora kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini.

**Kwa upande wake Rais wa TAHLISO Frank Nkinda aliishukuru HESLB kwa namna inavyoshughulikia kwa haraka masuala ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na kushauri kuendelea kushauriana na wadau mbalimbali wa elimu ili kuboresha mifumo ya kukabiliana na changamoto za wanafunzi kwa mwaka ujao wa masomo.**




# HESLB, SATF
## ZAINGIA MAKUBALIANO

**Na Mwandishi Wetu,**
**Dar es Salaam**

Katika kutekeleza dhamira ya serikali ya kuhakikisha wanafunzi wahitaji wanaopata udahili katika taasisi za Elimu ya Juu nchini wanawezeshwa kupata mikopo ili kufikia malengo yao, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeingia katika makubaliano maalum ya kimkakati na 'Social Action Trust Fund' (SATF) ili kuweza kuwabaini wanafunzi wahitaji wanaotoka kwenye kaya masikini au mazingira magumu na kuwawezesha kugharimia masomo yao ya elimu ya juu.

Akizungumza katika hafla ya kusaini makubaliano hayo iliyofanyika Januari, 31, 2023 katika ofisi za SATF Jijini Dar es salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul-Razaq Badru alisema dhamira ya Serikali ni kuhakikisha wanafunzi wote wanaopata udahili katika taasisi za Elimu ya Juu nchini na ambao wanapata ufadhili kutoka SATF wanapata mikopo kwa kiwango cha kutosheleza ili kutimiza ndoto zao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa SATF, Beatrice Mgaya alisema taasisi hiyo itahakikisha inasimamia kwa umakini malengo ya ushirikiano huo ili kuwezesha wanafunzi wahitaji wanaotoka katika kaya maskini au mazingira magumu wanapata mikopo ya elimu ya juu kupitia HESLB.

Malengo ya makubaliano hayo yaliyofikiwa kati ya HESLB na SATF ni kurasimisha uhusiano wa kimkakati kati ya taasisi hizo mbili kwa kuweka utaratibu wa kubadilishana taarifa na mifumo ya utambuzi ili kuwabaini waombaji mikopo wanaotoka kwenye mazingira magumu na ambao walipata ufadhili kutoka SATF katika masomo ya sekondari na hivyo kuwapatia mikopo ili kupata Elimu ya Juu.

Moja ya vigezo vya mwombaji mhitaji wa mikopo vilivyomo katika Sehemu ya 3.1 ya Mwongozo wa Utoaji Mikopo na ruzuku kwa mwaka wa masomo 2022/2023 inamtambua mwombaji anayetoka kwenye familia ya kipato cha chini au kaya maskini ambaye elimu yake ya sekondari au Stashahada (Diploma) alifadhiliwa na taasisi inayotambulika, kikundi cha kijamii au watu binafsi ambao wanatakiwa kuthibitisha ufadhili huo.

Waombaji wa aina hii wanatakiwa kupakua fomu ya ufadhili (SCSF-3) kutoka katika tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz) ambayo itajazwa na kuthibitishwa na taasisi mfadhili na kisha kuambatanishwa na nyaraka nyingine za maombi ya mkopo katika mtandao.

SATF ni shirika lisilo la kiserikali lililoanza kazi zake hapa nchini Tanzania mwaka 1998 likiwa na lengo la kusaidia watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu ikiwemo kuwawezesha kupata elimu kuanzia ngazi ya elimu ya awali.

**Moja ya vigezo vya mwombaji mhitaji wa mikopo vilivyomo katika Sehemu ya 3.1 ya Mwongozo wa Utoaji Mikopo na ruzuku kwa mwaka wa masomo 2022/2023 inamtambua mwombaji anayetoka kwenye familia ya kipato cha chini au kaya maskini ambaye elimu yake ya sekondari au Stashahada (Diploma) alifadhiliwa na taasisi inayotambulika, kikundi cha kijamii au watu binafsi ambao wanatakiwa kuthibitisha ufadhili huo.**

# WAZIRI MHAGAMA:

## TUMIENI MIFUMO KUBADILISHANA TAARIFA




**Na Mwandishi Wetu,**
**Arusha**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mheshimiwa Jenista Mhagama amesema upo umuhimu mkubwa wa kuongeza ufanisi wa utoaji huduma kwa umma na kubadilishana taarifa miongoni mwa taasisi za umma kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

Waziri Mhagama aliyasema hayo Februari 10, mwaka huu wakati akifunga Kikao Kazi cha Tatu cha Mwaka cha Serikali Mtandao kilichofanyika Jijini Arusha kwa siku tatu kuanzia Februari 8, 2023 na kuzihimiza taasisi zote za umma kujiunga kwenye Mfumo wa kubadilishana taarifa serikalini.

"Kutokana na umuhimu wa Taasisi za Umma kubadilishana taarifa, nina imani kuwa baada ya kutamatika kwa Kikao Kazi hiki, Taasisi zote ambazo bado hazijajiunga na Mfumo wa kubadilishana taarifa serikalini (Gov-ESB) zitafanya hivyo, ili kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa baina ya Taasisi za Umma na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma".

Katika kikao hicho pia, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) Abdul-Razaq Badru alipata fursa ya kuwasilisha mada kuhusu matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma HESLB ambapo alisema HESLB imepiga hatua kubwa katika matumizi ya TEHAMA katika kipindi cha miaka 17 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2005.

"Mwaka 2005 hadi 2010, tulikuwa tunachapisha fomu na kusambaza ili waombaji mkopo wajaze na kurejesha na waajiri walikua wanatulipa kwa hundi … utaratibu huu ulikuwa na changamoto nyingi," alibainisha Badru katika mkutano huo uliokua na washiriki zaidi ya 1,600.

Mkurugenzi Msaidizi wa TEHAMA wa HESLB, Bahati Singa ambaye pia alishiriki kwenye kikao kazi hicho cha Serikali Mtandao amesema, kwa sasa HESLB inafanya kazi kwa ukaribu sana na e-GA ili kuwa na mfumo jumuishi wa utoaji huduma serikalini. "Kufanya kazi na e-GA kumerahisisha uunganishaji wa mifumo na wadau muhimu na hivyo kusaidia huduma kuwafikia watanzania kwa haraka na ufanisi zaidi", amesema Singa.

Kikao hicho kilichowakutanisha washiriki 1,624 kutoka taasisi zaidi ya 380 za umma na binafsi kiliongozwa na kauli mbiu isemayo "Mifumo Jumuishi ya TEHAMA kwa Utoaji Bora wa Huduma kwa Umma".

Malengo makuu ya kikao hicho ambacho hufanyika mara moja kwa mwaka ni kuimarisha jitihada mbalimbali za kukuza Serikali Mtandao na kuhimiza mashirika ya serikali kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kuboresha utoaji huduma za umma, pamoja na kuwaunganisha wadau wakuu wa Serikali ili kujadili masuala mbalimbali TEHAMA na kushauriana juu ya namna bora ya kukabiliana na changamoto ambazo taasisi za umma hukabiliana nazo wakati wa kutekeleza majukumu yao.

# WADAU KUONGEZEKA UGHARIMIAJI ELIMU




**Na Mwandishi Wetu,**
**Dodoma**

HESLB imo mbioni kuboresha eneo la utoaji na urejeshaji mikopo kwa kuhusisha wadau wengi zaidi ili kuufanya mfuko wa mikopo kuwa stahimilivu na himilivu.

Katika kufikia azma hiyo, hivi karibuni HESLB iliandaa kongamano la kwanza na kuwashirikisha wadau wa ugharimiaji wa elimu ya juu nchini ambao wamebainisha umuhimu wa kuwepo kwa vyanzo vingi vya ughariamiaji wa elimu katika ngazi hiyo badala ya kutegemea serikali peke yake.

Hoja na michango ya wadau hao zilipatikana katika Kongamano la kwanza la Ugharimiaji wa Elimu ya Juu nchini lililoandaliwa na HESLB na kufanyika Machi 16, 2023 katika Hoteli ya Mtakatifu Gaspar Jijini Dodoma.

Kongamano hilo lililoongozwa na kauli mbiu isemayo "Tafakuri ya Ugharimiaji wa Elimu ya Juu nchini", lilijumuisha wadau zaidi ya 120 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (Zanzibar), Wizara ya Fedha na Mipango, Shirikisho la Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Vyuo Vikuu, taasisi za fedha na mashirika yasiyo ya serikali kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Awali akifungua kongamano hilo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Franklin Rwezimula alisema tafakuri kuhusu mfumo wa sasa wa ugharimiaji ni muhimu kwa kuwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya juu inaongezeka kila mwaka.

"Ni matumaini yangu kuwa majadiliano na tafakuri kutoka katika mkutano huu yatatoa mchango muhimu katika safari yetu ya kubadilisha mpango wa ufadhili wa elimu ya juu", alisema Dkt. Rwezimula.

Katika salamu za utangulizi, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB Prof. Hamisi O. Dihenga alisema katika miaka 18 ya kuwepo kwa HESLB kumekuwa na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu huku serikali ikiwa ni mfadhili mkuu na akaongeza kwamba ipo haja kwa HESLB kufanyia kazi mawazo mengi mazuri ya wadau bila kusubiri Kongamano lijalo.

Licha ya hotuba ya Mgeni Rasmi, mijadala ya wadau ilijikita katika mada tatu zilizowasilishwa na wasomi waliofanya utafiti na kutathmini athari za ongezeko la wanafunzi wa elimu ya juu kutokana na elimu bila ada shule za msingi na sekondari, umuhimu wa vyanzo vingine vya ughariamiaji kulingana na vipaumbele, na muundo wa kugharimia elimu ya juu kwa kuongeza vyanzo vya ziada ikiwemo mifuko ya hifadhi za jamii na benki.

Viongozi wengine walioshiriki ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (ZHELB) Prof. Mohammed Hafidh Khalfan, Mkurugenzi wa Elimu ya Juu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt Kennedy Hosea na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru.

Kongamano hilo lilifanyika kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) wa miaka mitano (2021-2026) unaolenga kuboresha elimu ya juu nchini kwa kuimarisha miundombinu, kujenga uwezo wa watendaji na mifumo ya TEHAMA.

HESLB Loans Board
INVESTING IN THE FUTURE

# Strategic Plan 2022/2023 - 2026/2027

# WE VALUE

## VISION

To become a reliable and sustainable Tanzanian financier for tertiary education students.

## MISSION

To sustainably issue loans and grants to eligible Tanzanians pursuing tertiary education & prudently manage loans collection.

## STRATEGIC THEMES

- Optimal lending and loan collection
- Business re-engineering and automation
- Strategic partnerships

## CORE VALUES

### ACCOUNTABILITY
We take the initiative to own our responsibilities by pursuing excellence, honouring our commitments and upholding integrity.

### CUSTOMER – CENTRIC
We are committed to prioritize and timely serve, listen and respond to customers' needs.

### TEAMWORK
We embrace networking and support one another in pursuit of excellence in serving customers.

### PROFESSIONALISM
We are qualified, skilled and passionate in delivering our services in accordance with highest standards of ethics.

### INNOVATION
We constantly develop solutions to address new lessons to meet the evolving needs of our customers.

### EQUITY
We treat our customers with fairness and respect to promote diversity and inclusion.

HESLB Tanzania | HESLB_Tanzania | 0739 665 533

## OUR PROJECT: Higher Education for Economic Transformation

HEET | WORLD BANK GROUP

**Description:**

- HEET is a USD. 4 million, five-year (2021/22 – 2025/26) project funded by the World Bank to promote reforms and improved operational capacity and delivery at HESLB.

  The project is steered by the Ministry of Education, Science and Technology
- **Project Development Objective:**
  To strengthen the learning environments and labor market orientation of programs in priority disciplines and the management of the higher education system
- **Component 2:**
  Strengthening the management of the higher education system

**Project Focus Areas**

- Business process re-engineering
- Performance and operational improvements on loans management
- Strengthening coordination and linkages with stakeholders
- Capacity building of staff
- Public-private partnerships
- Developing new policies to support equity, quality and sustainability.

## OUR CONTACT

### DAR ES SALAAM
HESLB House, 1 Kilimo Street, Tazara Area, Mandela Road,
P.O Box 76068, 15471 Dar es salaam, Tanzania
+255 739 665 533
info@heslb.go.tz

### DODOMA
PSSSF Building, Makole Road,
Plot No. 4&5, Block W. Uhindini Area,
+255 758 067 577 | +255 739 067 57
dodoma@heslb.go.tz

### ZANZIBAR
Michenzani Mall Building,
Michenzani Area, Side A,
5th Floor, Hall 501
P.O. Box 900
Zanzibar, Tanzania
+255 779 321414
zanzibar@heslb.go.tz

### MBEYA
CAG Building, Mbalizi Road
P.O. Box 319
Mbeya, Tanzania
0738 131310
0738 131311
mbeya@heslb.go.tz

### ARUSHA
NSSF Mafao House, 1st Floor,
P.O Box 2712,
Arusha, Tanzania
+255 27 2520128
+255 624 100011
+255 0739 102016
arusha@heslb.go.tz

### MTWARA
NHC Raha Leo Complex
2nd floor Plot no. 217 Block H.
Near Regional Commissioner's Office
P.O.Box 969,
Mtwara, Tanzania
Cell: 0736 026 668
mtwara@heslb.go.tz

### MWANZA
PSSSF Plaza Building, 2nd Floor
Front Wing, Kenyatta Road,
P.O. Box 3051,
Mwanza, Tanzania
+255 28 2506008
+255 759 819350
+255 738 153661
mwanza@heslb.go.tz

### CUSTOMER CENTRE
PSSSF Twin Towers,
Ground Floor,
Plot 120/121, Mission Street,
P.O. Box 76068,
Dar es salaam.